

SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 2
SOUAHÉLI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 2
SWAHILI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 2

Wednesday 22 May 2002 (morning)
Mercredi 22 mai 2002 (matin)
Miércoles 22 de mayo de 2002 (mañana)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied. Substantial references to a Part 2 work of the same genre are permissible but only in addition to the minimum of two Part 3 works. References to other works are permissible but must not form the main body of your answer.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- Ne pas ouvrir cette épreuve avant d'y être autorisé.
- Traiter un seul sujet de composition. La composition doit être basée sur au moins deux des œuvres étudiées dans la troisième partie du cours. La composition peut comporter des références importantes à une œuvre du même genre étudiée dans la seconde partie, mais uniquement en plus des deux œuvres de la troisième partie. Les références à d'autres œuvres sont permises mais ne doivent pas constituer l'essentiel de la réponse.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Elija un tema de redacción. Su respuesta debe basarse en al menos dos de las obras estudiadas para la Parte 3. Se podrán hacer referencias importantes a una obra de la Parte 2 del mismo género pero solamente como complemento a las dos obras de la Parte 3. Se permiten referencias a otras obras siempre que no formen la parte principal de la respuesta.

Andika insha juu ya moja ya masuala yafwatayo. Jibu lako lazima liwe juu ya angalau kazi mbili za sehemu ya 3 ulizojitayarisha nazo. Lazima uingize katika jibu lako mjadala wa kazi ya sehemu ya 2 ya utanzu huohuo mmoja kama inavyohusika. Majibu ambayo hayaegemei kwenye mjadala wa angalau kazi mbili za sehemu ya 3 hayatapata alama za juu.

Tamthilia

1. Ama

- (a) Katika kazi angalau mbili ulizosoma katika sehemu hii, onyesha jinsi wahusika wakuu wanavyoikabili migogoro inayosimuliwa.

Au

- (b) Linganisha kipengele cha lugha ya mazungumzo ya wahusika katika kazi mbili ulizosoma na useme kwa nini unadhani waandishi wake wamefaulu au kushindwa kujenga mazungumzo hayo.

Riwaya

2. Ama

- (a) Linganisha vipi riwaya mbili zilivyojengwa kutiririka kiwakati katika ploti zao.

Au

- (b) Elezea vipi kipengele cha mazingira ni muhimu kwa dhamira za angalau kazi mbili za sehemu hii ulizosoma.

Ushairi

3. Ama

- (a) “Sifa moja kuu ya fasihi ni kwamba hubadilika kutokana na kuathiriwa na wakati, siasa, utamaduni n.k.” Kwa kutumia mashairi machache ya washairi wawili kazi zao ulizosoma katika sehemu hii, jadili mabadiliko yao na vipi mabadiliko hayo yanaathiri usomaji wa maishairi yao.

Au

- (b) “Jinsi sauti ya mshairi inavyojieleza kwa hisia fulani na jinsi inavyolijenga shairi kimaana na kisanaa, ndiyo mambo muhimu yanayofanya shairi liwe na nguvu za kuvutia.” Kwa kurejelea kazi alizojitayarisha nazo katika sehemu hii jadili kwa kiasi gani kauli hii ina ukweli.

Riwaya ya Mapenzi

4. *Ama*

- (a) “Riwaya za mapenzi kila siku zinaonyesha jinsi jamii zinavyowaangalia kwa jicho tofauti wanawake na wanaume.” Kwa kupitia kazi mbili ulizosoma katika sehemu hii, jadili kwa kiasi gani unakubaliana na kauli hii.

Au

- (b) “Kipengele cha chuku au utiaji chumvi hutawala katika riwaya za mapenzi.” Je, unakubaliana na wazo hili? Jadili huku ukitoa mifano kutoka katika angalau kazi mbili ulizosoma katika sehemu hii.

Masuala ya Ujumla

5. *Ama*

- (a) “Fasihi haipo kwa kuakisi matatizo tu, bali ipo pia kwa kuburudisha.” Kwa kutumia mifano miwili onyesha uzani wa mambo haya mawili unavyowekwa na maandishi wake.

Au

- (b) Katika kazi mbili za fasihi ulizozisoma, onyesha vipi maandishi wake walivyofanikiwa au kutofanikiwa kukushawishi kifikra na kuvutia kimtindo katika maandishi yao.

Au

- (c) Kwa kutumia mifano ya kazi mbili za fasihi ulizosoma, onyesha vipi na kwa kiasi gani tamathali za semi ni mbinu muhimu katika fasihi.

Au

- (d) “Mtindo ni mwandishi mwenyewe na jinsi anavyoitumia lugha.” Jadili huku ukitoa mifano katika kazi mbili za fasihi ulizosoma.